
# IMANI ILIYOTAKATIFU SANA

## Somo la 7

**Neno lako ni kweli–Yohana 17:17**

*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# IMANI ILIYOTAKATIFU SANA

Katika somo lililopita tulijifunza kwamba imani ya Mkristo lazima ikue katika kile ambacho Biblia inakiita "Imani Iliyo Takatifu Sana" (Yuda 20). Hii ni imani yenye msingi wa mafundisho ya Biblia ambayo pekee ndiyo inaweza kuaminiwa kuwa ni kweli (Yohana 17:17). Leo tutajifunza "ukengeufu" kutoka kwenye Imani hii iliyo Takatifu Sana pamoja na ujuzi wa Biblia katika Kanisa na jinsi ungekeufu huo ulivyochukua nafasi.

Tunaanza na maneno haya kutoka kwa Mtume Paulo: "*Lakini nachelea; kama yule nyoka alivyomdanganya Eva kwa hila yake, asije akawaharibu fikira zenu, mkauacha unyofu na usafi kwa Kristo*" (2 Wakorintho 11:3 [1]). Paulo aliogopa kwamba kanisa lingedanganywa kama Hawa alivyodanganywa katika Edeni.

Ijapokuwa Adamu na Eva walizaa jamii ya binadamu, waliileta jamii hiyo katika "mauti" kama tunavyosoma hivi: "*Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi*" (Warumi 5:12). Lakini kwa wakati wake kutakuwa na "Adamu wa pili": "*ndivyo ilivyoandikwa, Mtu wa kwanza, Adamu, akawa nafsi iliyo hai; Adamu wa*

[1] Nukuu zote za Maandiko zimetoka katika *Toleo Mpya la Kimataifa* la Biblia.

*mwisho ni roho yenye kuhuisha*" (1 Wakorintho 15:45). Na pia kutakuwa na Eva wa pili, Kanisa, bibi-arusi wa Kristo.

Shetani anaendelea kudanganya kanisa kwa kuanzisha mafundisho ya uongo kama alivyofanya kwa Eva katika bustani ya Edeni. Mwanzoni mwa mojawapo ya barua zake, Paulo aliandika hivi: "*Enyi Wagalatia msio na akili! Nani aliyewaloga?*" (Wagalatia 3:1). Mtume aliwakemea ndugu katika kanisa hili juu ya suala la kushika Sheria ya Kiyahudi (sheria ya Musa). Swali hilo lilizua mkanganyiko mkubwa katika kanisa la kwanza. Kwa kuwa Wakristo wa kwanza walikuwa Wayahudi wote na walitoka kwenye mapokeo ya kushika kabisa torati na namna zake zote za ibada, hivyo kulikuwa na maoni mawili baina ya ndugu: kuendelea kushika, au kutoishika torati. Mfano: "*Wakashuka watu waliotoka Uyahudi wakawafundisha wale ndugu ya kwamba, Msipotahiriwa kama desturi ya Musa hamwezi kuokoka*" (Matendo 15:1).

Kwa hiyo, ilikuwa inaeleweka kwamba Wakristo wa kwanza wa kiyahudi hawakuwa na uhakika ikiwa walipaswa kuendelea kushika sheria ya Musa baada ya kuwa Wakristo. Shetani alitafuta kuwavuruga zaidi. Shetani hata alizusha shaka juu ya ufufuo: "*Lakini ikiwa inahubiriwa ya kwamba Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, wawezaje baadhi yenu kusema kwamba hakuna ufufuo wa wafu?*" (1 Wakorintho 15:12). Shetani alikuwa anajaribu kubatilisha injili ya "Kristo Aliyefufuka" katika siku za mwanzo za kanisa.

Bwana wetu Yesu na mtume Paulo walionya kuhusu udanganyifu huo na wadanganyifu hao: "*Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao*" (Matendo 20:29,30). Hapa mtume Paulo anazungumza juu ya manabii wa uongo walio kama "mbwa mwitu" ambao wangewinda kondoo. Yesu alitoa onyo kama hilo: "*Jihadharini*

*na manabii wa uwongo. Wanawajia wamevaa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali*" ( Mathayo 7:15 ). "Mavazi ya kondoo" yanawakilisha kifuniko cha nje cha fadhili na upole, lakini moyoni nia za manabii hao wa uongo ni tofauti kabisa. Mbwa mwitu daima anataka kula kondoo!

Tunaambiwa: "*Msujudie Mungu! Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii* " (Ufunuo 19:10). Kwa kuwa "ushuhuda wa Yesu" ni "roho ya Unabii," hivyo wale wanaoweza kueleza na kufundisha maandiko ni manabii na walimu wa kweli. Lakini Yesu alionya juu ya walimu wa uongo ambao walikuwa na kifuniko cha nje cha upole na fadhili lakini ambao kwa kweli walikuwa wakitafuta faida yao binafsi, waliharibu maisha ya kiroho ya kundi. Mtume Yohana alituonya hivi: "*Wapenzi, msiiamini kila **roho**, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wengi wametokea duniani. Katika hili mwaijua Roho ya Mungu; kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo alikuja katika mwili yatokana na Mungu* " (1 Yohana 4:1,2).

Yohana anasema tunapaswa "kuzijaribu roho." Katika Biblia neno "roho" kimsingi hurejelea kile kisichoonekana na chenye nguvu sana; Neno roho ina maana tatu kama zinavyoonekana hapa chini:

1. "**Pumzi ya uhai**" ambayo huhuisha na kudumisha uhai katika mwili "*Na **roho** humrudia Mungu aliyeitoa*" (1 Mhubiri 12:7). "Roho" hii haionekani na ina nguvu.

2. **Nia(Fikra)**: "*Nebukadreza akaota ndoto, **roho** yake ikafadhaika, usingizi wake ukamwacha*" (Danieli 2:1) "Roho" inarejelea nia(mawazo/fikra), na neno hilo ***mawazo*** limetumika katika tafsiri ya *TJK*. Nia haionekani na ina nguvu.

3. **Mafundisho**: "*Maneno niliyowaambia ni **roho** na ni uzima*" (Yohana 6:63). Hii ndiyo maana ya "roho" katika 1 Yohana 4:1,2. Mtume

Yohana alituonya tusiamini kila fundisho bali tujaribu kwa kutumia Neno la Mungu. Tunapaswa kuwa kama Waberoya waungwana: "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo* " (Matendo 17:11) ). Mfano gani wa uaminifu kwa kweli ulioonyeshwa na hawa Waberoya katika kanisa la kwanza!

Akizungumzia matukio ya baadaye ndani ya kanisa mtume Paulo aliandika: "*Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani*" (1 Timotheo 4:1,2). Chini ya uvuvioo wa roho mtakatifu mtume Paulo alitoa unabii kuhusu hali ndani ya kanisa la kristo karne mbili au tatu baadaye. Huo ulikuwa wakati ambapo Wakristo fulani 'waliiacha imani' na kuanza kuamini "roho zidanganyazo" (mafundisho ya kuvutia na ya kudanganya), "mambo yanayofundishwa na mapepo" (imani za kipagani), "waongo wanafiki," "wakikataza watu kuoa;" na "kujiepusha na vyakula fulani." Mafundisho haya yote yalitokea katika Kanisa la Kirumi la Kikatoliki. Mafundisho yasiyo ya kimaandiko yalihubiriwa na kukubaliwa. Ukuhani ulihitajika kuchukua nadhiri za usafi wa kiadili (kutokuoa) ingawa maandiko yanafundisha kinyume kabisa: "*Basi, imempasa Mwangalizi awe mtu asiye na lawama, mume wa* ***mke mmoja, mwenye kiasi, anayejitawala****, mwenye kustahiwa, mkarimu, awezaye kufundisha*" (1 Timotheo. 3:2). Baadaye Wakatoliki waaminifu waliambiwa hawawezi kula nyama siku ya Ijumaa, jambo ambalo halijafundishwa katika maandiko. Hivyo ulitimia unabii wa Paulo kuhusu kanisa na maendeleo yake ya baadaye.

Katika waraka wake wa pili kwa Timotheo, Paulo aliandika hivi: "*Hubiri Neno; kuwa tayari wakati ufaao na usiofaa; karipia, kemea na utie moyo – kwa uvumilivu wote na kwa mafundisho mazuri. Kwa maana utakuja wakati ambapo watu hawatakubali mafundisho yenye uzima. Badala yake, ili*

*kuptimiza na tamaa zao wenyewe, watajikusanyia idadi kubwa ya waalimu wapate kuwaambia yale ambayo masikio yao yanayowasha yanatamani kuyasikia. watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo*" ( 2 Timotheo 4:2-4 ). Huu ni unabii sawa na huo kuhusu wakati ambapo kungekuwa na anguko kubwa kutoka katika kweli kwa kupendelea "hadithi" (mafundisho ya uongo). Lakini anawaambia Wakristo wote wa kweli "Hubiri Neno; uwe tayari wakati ufaao na usiofaa". Ni lazima mtu awe macho na tayari kutumikia kweli iwe inafaa kwetu au la, lakini sikuzote inapowafaa wengine.

Mahubiri yetu yanapaswa kuwa "kwa uvumilivu(saburi) wote na mafundisho mazuri." kweli lazima ilindwe kwa bidii na isemwe kwa upendo na subira. Kama mtume Paulo alivyoandika katika waraka mwingine: "*Tukiambiana kweli katika upendo, na kukua katika mambo yote hata tumfikie yeye aliye Kichwa, yaani, Kristo*" (Waefeso 4:15). Ni baada tu ya kifo cha mitume ndipo tunaona mwanzo wa udanganyifu na kuanguka kutoka katika Imani iliyo Takatifu Sana ambayo ni maarifa ya Biblia.

Shughuli za kanisa la kwanza la Kikristo zilijikita katika sehemu kuu tano:

1. Yerusalemu katika Israeli.

2. Antiokia katika Ugiriki ambapo jina Mkristo lilitumiwa kwa mara ya kwanza: "*Kwa muda wa mwaka mzima Barnaba na Sauli walikutana na kanisa na kufundisha umati mkubwa wa watu. Wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza huko Antiokia*" (Matendo 11:26).

3. Alexandria huko Misri Kaskazini.

4. Konstantinopo nchini Uturuki.

5. Rumi nchini Italia.

Kanisa lilikuwa na “waangalizi” waliosimamia mafundisho na mambo ya kanisa. Kama ambavyo tumeona, mwangalizi alipaswa kuwa na mke mmoja tu. Hii ilikuwa nafasi ya juu kabisa ndani ya kanisa. Kungekuwa na waangalizi tofauti kwa maeneo na miji tofauti. Hawa wanaweza kuja pamoja mara kwa mara ili kujadili ustawi wa kanisa kwa ujumla. Mtume Yohana na mtume Paulo walitumikia wakiwa waangalizi. Hakuna waliopewa vyeo maalum. Lakini katika makanisa ya leo, kuna majina mbalimbali ya vyeo, ambayo maarufu zaidi ni “Wa kuogopwa.”

Mtunga-zaburi anatuambia ni nani pekee anayepaswa kuwa na cheo hiki: “Aliwapelekea watu wake ukombozi **;** Mtakatifu na **Wa kuogopwa** ndilo jina lake” (Zaburi 111:9 *)* . Ni Mungu mkuu mweza yote mwenyewe ambaye ni “wa kuogopwa.” TJK *inatumia* neno "kutisha/kustaajabisha" kutafsiri Kiebrania. Tunapotazama kazi za uumbaji zisizo na kikomo za Mungu, tunapata uumbaji wenyewe kuwa "wa kustaajabisha"! Cha kustaajabisha zaidi ni muumbaji wake – yaani Mungu! ***Hakuna mwanadamu anayepaswa kuchukua cheo kilichowekwa kwa ajili ya Mungu***.

Yesu alituambia, “*Msimwite mtu yeyote baba duniani, kwa maana mna Baba mmoja, naye yuko mbinguni*” (Mathayo 23:9). Hata hivyo, licha ya ombi hili la wazi, makasisi wa Kikatoliki wa Kirumi wanatarajia kuitwa “Baba” na Wakatoliki waaminifu.

Maandiko yanatuambia Yesu ni "kichwa juu ya kila kitu kwa ajili ya kanisa": "*Naye Mungu ameweka **vitu** vyote viwe chini ya miguu yake, na akamweka yeye awe kichwa juu ya **vitu vyote** kwa ajili ya kanisa, ambalo ni mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa kila kitu kwa kila namna*” (Waefeso 1:22,23). Hivyo madai ya Papa kuwa “kichwa” cha kanisa ni uongo.

Kanisa Katoliki la Kirumi linadai ukuu wa papa unaidhinishwa na maneno haya: "*Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu*" (Mathayo 16:18). Inadai Bwana wetu alimteua Petro kuwa "kichwa" cha Kanisa, papa wake wa kwanza kana kwamba ni jiwe la msingi! Hebu tuone kilichotokea kwa hili "jiwe la msingi" dakika chache baadaye: "*Yesu akageuka, akamwambia Petro, Nenda nyuma yangu, Shetani! Wewe ni kikwazo kwangu; huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu*" (Mathayo 16:23). Karibia papo hapo Bwana wetu anamrejelea huyu anayedhaniwa kuwa "kichwa" kipya cha kanisa lake kama "Shetani"!

Maneno ya Yesu kwa Petro hayana uhusiano wowote na kumfanya awe kichwa juu ya viongozi wengine wote wa kanisa. Hiki ndicho kilichotukia muda mfupi kabla ya Yesu kumwambia Petro maneno hayo: "*Basi Yesu alipofika katika eneo la Kaisaria-Filipi, akawauliza wanafunzi wake, "Watu husema kwamba Mwana wa Adamu ni nani?" Wakamjibu, "Baadhi husema ni Yohana Mbatizaji; wengine husema ni Elia; na bado wengine husema ni Yeremia au mmojawapo wa manabii." Akawauliza, "Je, ninyi mnasema mimi ni nani?" Simoni Petro akamjibu, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Naye Yesu akamwambia, "Heri wewe, Simoni Bar-Yona,kwa maana hili halikufunuliwa kwako na mwanadamu, bali na Baba yangu aliye mbinguni*" ( Mathayo 16:13-17 ).

Kwanza Yesu aliuliza swali: "Watu husema Mwana wa Adamu kuwa ni nani?" Majibu yalikuwa yametofautiana na ya mkanganyiko. Yesu alipowauliza wanafunzi wake maoni yao, mtume Petro ndiye aliyetoa jibu sahihi kwa uwezo wa roho takatifu! Baada ya kufanya hivyo, Yesu alisema: "Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu."

Jina Petro linatokana na neno la Kigiriki *petros* lenye maana ya ***jiwe dogo***. Neno "mwamba" linatokana na neno la Kigiriki *petra* ambalo

linamaanisha ***jiwe mkubwa*** au ***mwamba***. Kuna tofauti ya wazi ya maana kati ya maneno haya mawili. Yesu alimaanisha kwamba "mwamba" ambao angejenga kanisa lake juu yake ulikuwa ni kweli (neno la Mungu): "*kama nikikawia, utajua jinsi iwapasavyo watu kuenenda katika nyumba ya Mungu, ambayo ndiyo kanisa la Mungu aliye hai, lililo nguzo na msingi wa* ***kweli***" (1 Timotheo 3:15). Msingi ni Yesu Kristo mwenyewe: "*Kwa maana hakuna mtu awezaye kuweka msingi mwingine isipokuwa ule uliokwisha kuwekwa, ambao ni Yesu Kristo*" (Wakorintho 3:11). Yesu alijiita yeye mwenyewe kuwa "kweli": "*Mimi ndiye njia na kweli na uzima. mtu haji kwa Baba ila kwa njia ya mimi*" (Yohana 14:6).

Hivyo Yesu alikuwa anamwambia Petro kwamba yeye mwenyewe alikuwa msingi wa kanisa, si mtu mwingine, na kwa hakika si Petro. Walakini pasina shaka Petro pamoja na wengine kumi na mmoja ni jiwe la msingi la "Yerusalemu Mpya": "*Ukuta wa mji huo ulikuwa na misingi kumi na miwili, na juu yake kulikuwa na majina ya wale mitume kumi na wawili wa Mwana-Kondoo*" (Ufunuo 21:14).

Kisha Yesu akamwambia Petro kwamba angempa jambo la pekee: "*Nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni, na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni*" (Mathayo 16:19). Hizi "funguo" kwa kawaida zinadaiwa na papa wa katoliki ya Kirumi kuwa ni funguo za mbinguni na kuzimu. Hapana kabisa! "Ufunguo" hutoa njia ya ama kufungua "mlango" wa fursa au wa *jambo. Wakati mwingine inawakilisha kupokea mamlaka kutoka kwa mwingine:* "*Nina funguo za mauti na kuzimu*" (Ufunuo 1:18). "Funguo" alizopewa Petro zilifungua mlango wa fursa ya kuwa mshirika wa kundi la ufalme. "Funguo" hizo mbili zilitumika kwa vikundi viwili tofauti:

**Kwa Wayahudi:** Mlango huu ulifunguliwa Siku ya Pentekoste, 33 BK (ona Matendo 2:14-41).

**Kwa Mataifa:** Mlango huu ulifunguliwa nyumbani kwa Kornelio, 36 AD
(ona Matendo 10:23-48).

Katika mifano/mafumbo mawili Bwana wetu alitabiri juu ya kile ambacho kingetokea kwa "ufalme wa mbinguni" wakati wa maendeleo yake katika enzi(zama) ya Injili. Hili ndilo fumbo la kwanza: "*Ufalme wa mbinguni umefanana na mbegu ya haradali ambayo mtu aliichukua na kuipanda katika shamba lake. Ijapokuwa ni ndogo kuliko mbegu zenu zote, lakini ikiisha kukua, huwa kubwa kuliko mimea yote ya bustani, huwa mti, hata ndege wa angani huja na kukaa katika matawi yake*" (Mathayo 13:31,32). Hii inawakilisha mwanzo mdogo wa kazi ya kuanzisha kanisa katika karne ya kwanza, na ukuaji wake wa baadaye katika karne zilizofuata. Sasa hebu tuzingatie undani wa fumbo hili:

**Mbegu ya haradali**—Kama vile mbegu ya haradali ni ndogo, kanisa la Kikristo lilikuwa na mwanzo mdogo na mitume kumi na wawili tu na wanafunzi wachache.

**Ambayo mtu alichukua** -Kazi ya kutangaza injili ya ufalme ilianza na Yesu; iliendelezwa na mitume na wanafunzi wake chini ya mamlaka yake (ona Matendo 1:8).

**Aliipanda katika shamba lake** —shamba ni ulimwengu (ona Mathayo 13:38). Na kwa hivyo kazi ya kutangaza injili ilienea ulimwenguni kote.

**Lakini inapokua** —Hii inawakilisha kupita kwa wakati jinsi kanisa lilivyokua katika karne zilizofuata. Kawaida mmea wa haradali hukua hadi urefu wa futi mbili hadi tatu. Lakini kwa hili kulikuwa na ukuaji usio wa kawaida. "Ikawa mti." Hivyo Ukristo ulikuwa na ukuaji usio wa kawaida na ukawa dini kubwa yenye washirika wengi sana.

**Ndege wa angani—** Shetani ndiye "mtawala wa ufalme wa anga" (Waefeso 2:2). "Ndege" ni watumishi wake, watu wenye nia ya kidunia wanaotafuta faida na heshima ya kidunia ndani ya mfumo wa kanisa.

**hukaa katika matawi** —Hawa watu wenye nia ya kiulimwengu walichukua nyadhifa muhimu za mamlaka na umuhimu ndani ya mfumo wa kanisa. Hii ni picha iliyo wazi ya kiunabii ya matawi mbalimbali ya Jumuiya ya Wakristo pamoja na madhehebu yake yapatayo takriban 750.

Kisha Yesu akatoa fumbo/mfano wa pili: "*Ufalme wa mbinguni umefanana na chachu ambayo mwanamke aliitwaa na kuichanganya katika unga mwingi mpaka unga wote ukaumuka*" (Mathayo 13:33). Sasa hebu tuzingatie undani wa fumbo/mfano huu:

**Chachu** —hii ni ishara ya mafundisho ya uongo. "*Jihadharini na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo*" ( Mathayo 16:11 ) Haya ni baadhi ya mafundisho ya Masadukayo: "*Masadukayo husema kwamba hakuna ufufuo, na kwamba hakuna malaika wala roho*" (Matendo 23:8).

**Mwanamke aliitwaa**—"mwanamke" katika Biblia anaweza kuwa ishara ya kanisa, bibi-arusi wa wakati ujao wa Kristo: "*Ninawaonea wivu, wivu wa Kimungu, kwa kuwa mimi niliwaposea mume mmoja, ili niwalete kwa Kristo kama bikira safi*" (2 Wakorintho 11:2). Lakini katika mfano huo mwanamke si mzuri. Ni kanisa la uongo lililotajwa katika Ufunuo 17:1, 2 ambalo wafalme wa dunia wamefanya uzinzi nalo.

**Kiasi kikubwa cha unga** —Hii inawakilisha chakula safi kinachotolewa na Bwana kwa ajili ya nyumba ya imani. "Unga" huo uliharibiwa kwa utaratibu na chachu ya mafundisho ya uongo na hatimaye kuharibika. Kujifunza Biblia kulipuuzwa huku imani za kilimwengu zikiingia kanisani taratibu. Kweli za Biblia zilianza


kutoweka. Mamlaka za kanisa zilianza kutawala na kutafuta heshima duniani. Tumaini lenye baraka la kuteseka **sasa** ili **baadaye** kutawala pamoja naye likaharibika. Mfano huo unaonyesha jinsi kanisa lingepoteza kweli inayoelezwa katika Neno la Mungu.

Isaya anaeleza hali ya sasa ya kanisa la Kikristo: "*Watu hawa hunikaribia kwa vinywa vyao na kuniheshimu kwa midomo tu, lakini mioyo yao iko mbali nami. Ibada yao kwangu inatokana na maagizo yanayofundishwa na wanadamu*" (Isaya 29:13).

Tunajua kusema kweli hakutakuwa maarufu. Haikuwa maarufu wakati mitume walipokuwa hai. Wayahudi wa Rumi walimwambia mtume Paulo hivi: "*Lakini tunataka kusikia kwako uonavyo wewe; kwa maana katika habari za dhehebu hilo imejulikana kwetu kwamba inanenwa vibaya kila mahali.*"( Matendo 28:22 ). Hiyo bado ni kweli hata leo.

Maadui wa Paulo walipomleta mbele ya Feliksi, walisema alikuwa "kiongozi wa dhehebu la Wanazorayo" (Matendo 24:5). Na leo wafuasi wa imani ya kweli, ile kweli, wanaitwa pia "dhehebu" au "dini." Lakini katikati ya mkanganyiko na mapotovu yote, waaminifu wa Mungu wanahakikishiwa upendo na mwongozo wake: "*Njia ya wenye haki ni kama nuru ya kwanza ya mapambazuko, ambayo hung'aa zaidi na zaidi mpaka mchana mkamilifu*" (Mithali 4:18)

**-Amina-**



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***